



**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**PATO LA TAIFA KWA MWAKA 2017**



**Ofisi ya Taifa ya Takwimu  
Wizara ya Fedha na Mipango  
Machi, 2018**

## **1.0 Utangulizi**

Pato la Taifa ni thamani ya bidhaa na huduma zinazozalishwa Nchini katika kipindi husika. Pato la Taifa hutumika kutathmini ukuaji wa uchumi katika mwaka husika. Taarifa hii ni kwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba, 2017.

Taarifa zilizotumika kutayarisha takwimu za Pato la Taifa kwa mwaka 2017 zimetokana na uzalishaji wa bidhaa na huduma Nchini katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2017 kutoka vyanzo mbalimbali vya takwimu rasmi kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali. Aidha, ukokotoaji wa takwimu za Pato la Taifa umezingatia matakwa ya Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 2008 (United Nations, System of National Accounts 2008).

## **2.0 Matokeo Muhimu**

Thamani ya Pato la Taifa kwa bei za soko za miaka husika katika mwaka 2017 iliongezeka na kufikia shilingi trilioni 116.1 kutoka shilingi trilioni 103.1 mwaka 2016.

Aidha, thamani ya Pato la Taifa kwa bei ya soko ya mwaka 2007 zilikuwa shilingi trilioni 50.5 mwaka 2017 kutoka shilingi trilioni 47.1 mwaka 2016, ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 7.1.

## **3.0 Ukuaji wa Shughuli za Kiuchumi**

Ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika mwaka 2017 unaonesha kuwa, shughuli zilizokua kwa kasi kubwa ni pamoja na Uchimbaji Madini na Mawe (asilimia 17.5), Usambazaji Maji (asilimia 16.7), Uchukuzi na uhifadhi Mizigo (asilimia 16.6), Habari na Mawasiliano (asilimia 14.7) na Ujenzi (14.1).

Muhtasari wa mchanganuo wa baadhi ya shughuli za kiuchumi katika mwaka 2017 ulikuwa kama ifuatavyo:

### **3.1 Kilimo, Mifugo, Misitu na Uvuvi**

Shughuli hizi zinajumuisha uvunaji wa mazao ya mimea, wanyama, uvunaji wa mazao ya miti kutoka katika mashamba ya miti na mazao ya miti ya porini na uzalishaji wa samaki na mazao ya samaki.

Mwaka 2017, ongezeko la thamani ya shughuli za kiuchumi za kilimo, mifugo, misitu na uvuvi kwa bei za mwaka 2007 iliongezeka na kufikia shilingi trilioni 10.3 kutoka shilingi trilioni 9.9 mwaka 2016 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 3.6.

#### **3.1.1 Kilimo cha Mazao**

Shughuli za mazao zinajumuisha uvunaji wa mazao ya mimea, na uvunaji wa mazao ya miti. Katika mwaka 2017, ongezeko la thamani ya shughuli za kilimo cha mazao iliongezeka na kufikia shilingi trilioni 5.3 kutoka shilingi trilioni 5.1 mwaka 2016 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 3.7. Ukuaji huu ulitokana na kupatikana kwa mvua za kutosha katika maeneo ya uzalishaji wa mazao.

Ukuaji wa shughuli ya mazao ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali kama vile mahindi kwa asilimia 8.7 kutoka tani elfu 6,149 mwaka 2016 hadi tani elfu 6,681 mwaka 2017, Mtama/Ulezi kwa asilimia 6.1 kutoka tani 1,003 mwaka 2016 hadi tani elfu 1,064 mwaka 2017. Maharage/ Mikunde uliongezeka kwa asilimia 18.3 kutoka tani elfu 1,959 katika mwaka 2016 hadi tani elfu 2,318 mwaka 2017. Viazi ( mviringo na vitamu) uliongezeka kwa asilimia 34.7 kutoka tani elfu 1,491 mwaka 2016 hadi tani elfu 2,008 mwaka 2017.

#### **3.1.2 Mifugo**

Uzalishaji wa mifugo na mazao yake unatokana na ufugaji wa mifugo ya kiasili na iliyoboreshwa. Mifugo hiyo ni pamoja na ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, punda, farasi, sungura na kuku.

Mwaka 2017, ongezeko la thamani ya shughuli za uzalishaji mifugo na mazao yake iliongezeka hadi shilingi trilioni 3.4 kutoka shilingi trilioni 3.3 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 2.8. Kasi ya ukuaji wa shughuli hii ilitokana na kuongezeka kwa idadi ya wanyama waliovunwa na pia kuongezeka kwa mazao ya wanyama ambayo ni pomaja na maziwa, ngozi na mayai.

### **3.1.3 Misitu**

Shughuli hii inahusika na uzalishaji wa mazao ya misitu ambayo ni magogo, mkaa, kuni, na mazao mengine ya misitu yasiyotokana na miti kama asali na nta.

Mwaka 2017, ongezeko la thamani ya shughuli za misitu lilikua hadi kufikia kiasi cha shilingi bilioni 957.8 kutoka shilingi bilioni 901.2 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 6.3.

### **3.1.4 Uvuvi**

Shughuli ya uvuvi inahusika na uvunaji wa rasilimali za baharini na maji baridi, kwa lengo la kuvua samaki na mazao mengine ya bahari.

Mwaka 2017, ongezeko la thamani ya shughuli za uvuvi lilikua hadi kufikia kiasi cha shilingi bilioni 575.2 kutoka shilingi bilioni 560.0 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 2.7. Ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa samaki waliovunwa pamoja na mazao ya samaki katika kipindi hicho.

## **3.2 Uchimbaji Madini na Mawe**

Uchimbaji madini na mawe unahusisha ukusanyaji wa madini yabisi yanayopatikana kwenye uso wa dunia (kama vile makaa ya mawe na chuma), vimiminika (petroli) au gesi (gesi asilia). Ukusanyaji huu unaweza kuwa chini ya ardhi, juu ya ardhi na pia kutoka kwenye visima. Shughuli hii inajumuisha pia kazi za ziada za kuongeza thamani ya madini kama vile kusafisha kukata na kupanga katika madaraja tayari kwa kupelekwa kwenye masoko.

Mwaka 2017, ongezeko la thamani la shughuli za uchimbaji madini na mawe lilikua hadi kufikia kiasi cha shilingi trilioni 1.98 kutoka shilingi trilioni 1.68 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 17.5.

Ukuaji wa shughuli hii ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa gesi asilia, almasi na makaa ya mawe. Aidha, uzalishaji wa makaa ya mawe uliongezeka kutokana na Serikali kuzuia uagizaji wa makaa ya mawe kutoka nje. Uzalishaji wa gesi asilia uliongezeka ili kukidhi mahitaji ya uzalishaji wa umeme na viwanda vipya vilivyounganishwa katika bomba la gesi. Kiasi cha baadhi ya madini yaliyozalishwa mwaka 2016 na 2017 kimeainishwa kwenye jedwali Namba 1.

**Jedwali Na.1: Uzalishaji wa Baadhi ya Madini kwa Mwaka 2016 na 2017**

Madini	Kipimo	2016	2017
Almasi	Karati	216,023	304,456
Gesi Asilia	Futi Ujazo Milioni	45,518	52,248
Makaa ya Mawe	Tani	275,307	558,553

Chanzo: Wizara ya Madini 2018

### **3.3 Uzalishaji Bidhaa Viwandani**

Ongezeko la thamani la shughuli za utengenezaji bidhaa viwandani lilikua hadi kufikia shilingi trilioni 3.719 mwaka 2017 kutoka shilingi trilioni 3.473 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 7.1.

Kasi ya ukuaji ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za vyakula; kemikali na simenti; na bidhaa za mbao na karatasi.

### **3.4 Ujenzi**

Ongezeko la thamani la shughuli ya ujenzi lilikua hadi kufikia kiasi cha shilingi trilioni 6.159 mwaka 2017 kutoka shilingi trilioni 5.396 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 14.1.

Ongezeko hili lilitokana na ujenzi wa majengo ya biashara na makazi pamoja na miradi ya ujenzi wa miundombinu

inayoendelea kujengwa Nchini kama vile ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), upanuzi wa uwanja wa ndege wa Mwanza, ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Ubungo na TAZARA Jijini Dar es Salaam, ujenzi wa barabara ya Manyoni – Tabora, na barabara nyingine katika kiwango cha lami Nchini.

### **3.5 Elimu**

Shughuli hii inahusika na utoaji wa elimu katika ngazi mbalimbali za taasisi za binafsi na za umma. Katika mwaka 2017 ongezeko la thamani la shughuli ya elimu lilikua hadi kufikia kiasi cha shilingi trilioni 1.672 kutoka shilingi trilioni 1.541 mwaka 2016 sawa la ongezeko la asilimia 8.5. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa wanafunzi waliodahiliwa katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya elimu ya juu. Halikadhalika, utekelezaji wa Sera ya Elimumsingi bila malipo imeendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la udahili wa wanafunzi.

### **3.6 Afya**

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa huduma za afya ya binadamu na ustawi wa jamii kwa watoa huduma binafsi na umma.

Ongezeko la thamani la shughuli hii lilikua hadi kufikia shilingi bilioni 828.0 mwaka 2017 kutoka shilingi bilioni 781.6 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 5.9. Ukuaji huu ulitokana na Serikali kuongeza fedha za ununuzi wa vifaa tiba na madawa Nchini.

## **4.0 Hitimisho**

Pato la Taifa limetayarishwa kutokana na taarifa zilizokusanywa kutoka katika shughuli za kiuchumi katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2017. Ukuaji wa Pato la Taifa kwa kiwango cha asilimia 7.1 linaonesha mwelekeo chanya katika kufikia malengo ya Serikali ya kuwa Nchi yenye uchumi wa kati.

Majedwali ya ukuaji na mchango katika Pato la Taifa yameambatishwa.

**PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO  
(BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)**

Jedwali NA.1		Sh. Milioni										
SHUGHULI YA KIUCHUMI		2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017
A	<b>Kilimo, Misitu na Uvuvi</b>	<b>7,181,357</b>	<b>9,432,725</b>	<b>11,407,717</b>	<b>13,110,123</b>	<b>15,488,232</b>	<b>19,095,551</b>	<b>22,129,214</b>	<b>22,969,225</b>	<b>26,346,673</b>	<b>30,160,064</b>	<b>34,984,237</b>
	Kilimo cha Mazao	3,603,539	5,013,561	6,036,056	7,285,021	8,686,663	11,035,044	12,413,982	12,851,664	14,193,178	16,100,130	19,736,453
	Mifugo	2,513,284	3,062,768	3,643,718	3,968,924	4,572,949	5,194,037	5,839,240	5,843,715	7,135,172	7,962,471	8,019,826
	Misitu	639,762	752,278	881,217	956,104	1,146,811	1,507,793	2,167,981	2,492,043	3,146,646	4,041,455	4,651,478
	Uvuvi	424,772	604,118	846,726	900,074	1,081,809	1,358,678	1,708,011	1,781,803	1,871,677	2,056,008	2,576,480
	<b>Viwanda na Ujenzi</b>	<b>5,406,038</b>	<b>6,700,408</b>	<b>7,018,516</b>	<b>8,900,127</b>	<b>12,026,624</b>	<b>13,393,627</b>	<b>16,108,617</b>	<b>18,516,194</b>	<b>22,093,942</b>	<b>25,722,681</b>	<b>30,616,524</b>
B	Uchimbaji Madini na Mawe	935,412	991,017	1,073,019	1,779,711	2,688,584	3,001,179	2,986,466	2,923,420	3,659,599	4,975,991	5,560,120
C	Viwanda	1,880,032	2,283,594	2,597,316	3,021,536	4,031,541	4,599,919	4,575,334	4,445,568	4,768,917	5,070,871	6,412,042
D	Umeme	232,622	306,628	354,862	406,272	303,444	533,283	546,670	874,306	898,681	775,321	636,183
E	Maji safi na Maji taka	240,898	247,646	264,520	261,294	247,825	275,053	325,969	373,549	392,557	422,698	541,797
F	Ujenzi	2,117,074	2,871,523	2,728,799	3,431,314	4,755,231	4,984,193	7,674,179	9,899,350	12,374,188	14,477,799	17,466,382
	<b>Huduma</b>	<b>12,692,496</b>	<b>14,748,265</b>	<b>17,147,365</b>	<b>19,386,862</b>	<b>22,544,171</b>	<b>25,712,641</b>	<b>29,102,168</b>	<b>32,605,809</b>	<b>36,344,236</b>	<b>40,454,788</b>	<b>43,542,049</b>
G	Biashara na Matengenezo	2,645,347	3,193,697	3,744,883	4,426,467	5,571,372	6,389,279	7,271,716	8,378,449	9,714,665	11,091,210	12,784,878
H	Uchukuzi na Uhifadhi mizigo	1,572,854	1,969,499	2,320,841	2,537,407	2,728,970	2,733,618	2,986,347	3,438,077	3,864,482	4,480,106	4,941,814
I	Malazi na Huduma ya chakula	481,997	559,793	680,669	720,772	733,958	887,972	902,810	872,341	957,268	969,172	1,024,164
J	Habari na Mawasiliano	615,066	722,548	912,732	1,151,748	1,244,894	1,454,665	1,624,384	1,700,411	1,809,897	2,025,901	2,309,630
K	Fedha na Bima	756,075	959,279	1,178,853	1,408,477	1,772,783	2,070,163	2,308,705	2,694,444	3,254,440	3,731,191	3,846,713
L	Upangishaji Majengo	1,601,266	1,716,408	1,921,328	2,036,908	2,277,778	2,612,765	2,672,147	2,955,417	2,932,490	3,062,480	3,160,944
M	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi	318,677	450,188	552,630	728,207	813,502	810,126	902,695	1,003,126	1,103,124	1,228,052	1,285,562
N	Huduma zinazohusiana na Utawala	793,110	850,083	895,051	978,846	1,098,620	1,427,909	1,711,730	2,003,202	2,160,207	2,289,112	2,439,613
O	Utawala na Ulinzi	2,179,164	2,282,704	2,511,953	2,668,756	3,338,192	4,017,280	4,936,071	5,227,502	5,852,605	6,499,975	6,289,763
P	Elimu	851,208	1,007,308	1,193,228	1,380,170	1,463,767	1,607,317	1,893,665	2,172,080	2,309,345	2,425,025	2,529,286
Q	Afya na Huduma za Jamii	438,415	532,163	663,618	735,665	820,894	919,307	1,019,987	1,151,978	1,275,702	1,429,962	1,577,956
R	Sanaa na Burudani	91,527	105,579	114,977	125,499	144,046	169,112	188,996	221,912	241,508	275,199	303,968
S	Huduma nyingine za Kijamii	254,462	294,114	344,078	366,539	406,498	472,947	534,380	619,835	690,814	762,419	847,000
T	Shughuli za Kaya katika kuajiri	93,329	104,904	112,524	121,402	128,896	140,180	148,536	167,035	177,691	184,984	200,759
X	Ushuru wa Mabenki	-331,002	-289,027	-327,342	-376,200	-557,921	-638,332	-867,157	-826,396	-1,037,814	-1,082,044	-1,073,750
	<b>Jumla ya Ongezeko la Thamani</b>	<b>24,948,888</b>	<b>30,592,371</b>	<b>35,246,256</b>	<b>41,020,912</b>	<b>49,501,106</b>	<b>57,563,488</b>	<b>66,472,842</b>	<b>73,264,831</b>	<b>83,747,037</b>	<b>95,255,489</b>	<b>108,069,061</b>
	Ongeza kodi katika bidhaa	1,821,544	2,172,568	2,480,568	2,815,106	3,261,475	3,870,726	4,480,385	6,453,585	7,116,789	7,913,122	8,032,846
	<b>Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko</b>	<b>26,770,432</b>	<b>32,764,940</b>	<b>37,726,824</b>	<b>43,836,018</b>	<b>52,762,581</b>	<b>61,434,214</b>	<b>70,953,227</b>	<b>79,718,416</b>	<b>90,863,827</b>	<b>103,168,611</b>	<b>116,101,908</b>

**PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO  
(BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)**

Jedwali NA.2												Asilimia
<b>SHUGHULI YA KIUCHUMI</b>		<b>2007</b>	<b>2008</b>	<b>2009</b>	<b>2010</b>	<b>2011</b>	<b>2012</b>	<b>2013</b>	<b>2014</b>	<b>2015</b>	<b>2016</b>	<b>2017</b>
A	<b>Kilimo, Misitu na Uvuvi</b>	<b>26.8</b>	<b>28.8</b>	<b>30.2</b>	<b>29.9</b>	<b>29.4</b>	<b>31.1</b>	<b>31.2</b>	<b>28.8</b>	<b>29.0</b>	<b>29.2</b>	<b>30.1</b>
	Kilimo cha Mazao	13.5	15.3	16.0	16.6	16.5	18.0	17.5	16.1	15.6	15.6	17.0
	Mifugo	9.4	9.3	9.7	9.1	8.7	8.5	8.2	7.3	7.9	7.7	6.9
	Misitu	2.4	2.3	2.3	2.2	2.2	2.5	3.1	3.1	3.5	3.9	4.0
	Uvuvi	1.6	1.8	2.2	2.1	2.1	2.2	2.4	2.2	2.1	2.0	2.2
B	Uchimbaji Madini na Mawe	3.5	3.0	2.8	4.1	5.1	4.9	4.2	3.7	4.0	4.8	4.8
C	Viwanda	7.0	7.0	6.9	6.9	7.6	7.5	6.4	5.6	5.2	4.9	5.5
D	Umeme	0.9	0.9	0.9	0.9	0.6	0.9	0.8	1.1	1.0	0.8	0.5
E	Maji safi na Maji taka	0.9	0.8	0.7	0.6	0.5	0.4	0.5	0.5	0.4	0.4	0.5
F	Ujenzi	7.9	8.8	7.2	7.8	9.0	8.1	10.8	12.4	13.6	14.0	15.0
G	Biashara na Matengenezo	9.9	9.7	9.9	10.1	10.6	10.4	10.2	10.5	10.7	10.8	11.0
H	Uchukuzi na Uhifadhi mizigo	5.9	6.0	6.2	5.8	5.2	4.4	4.2	4.3	4.3	4.3	4.3
I	Malazi na Huduma ya chakula	1.8	1.7	1.8	1.6	1.4	1.4	1.3	1.1	1.1	0.9	0.9
J	Habari na Mawasiliano	2.3	2.2	2.4	2.6	2.4	2.4	2.3	2.1	2.0	2.0	2.0
K	Fedha na Bima	2.8	2.9	3.1	3.2	3.4	3.4	3.3	3.4	3.6	3.6	3.3
L	Upangishaji Majengo	6.0	5.2	5.1	4.6	4.3	4.3	3.8	3.7	3.2	3.0	2.7
M	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi	1.2	1.4	1.5	1.7	1.5	1.3	1.3	1.3	1.2	1.2	1.1
N	Huduma zinazohusiana na Utawala	3.0	2.6	2.4	2.2	2.1	2.3	2.4	2.5	2.4	2.2	2.1
O	Utawala na Ulinzi	8.1	7.0	6.7	6.1	6.3	6.5	7.0	6.6	6.4	6.3	5.4
P	Elimu	3.2	3.1	3.2	3.1	2.8	2.6	2.7	2.7	2.5	2.4	2.2
Q	Afya na Huduma za Jamii	1.6	1.6	1.8	1.7	1.6	1.5	1.4	1.4	1.4	1.4	1.4
R	Sanaa na Burudani	0.3	0.3	0.3	0.3	0.3	0.3	0.3	0.3	0.3	0.3	0.3
S	Huduma nyingine za Kijamii	1.0	0.9	0.9	0.8	0.8	0.8	0.8	0.8	0.8	0.7	0.7
T	Shughuli za Kaya katika kuajiri	0.3	0.3	0.3	0.3	0.2	0.2	0.2	0.2	0.2	0.2	0.2
X	Ushuru wa Mabenki	-1.2	-0.9	-0.9	-0.9	-1.1	-1.0	-1.2	-1.0	-1.1	-1.0	-0.9
	<b>Jumla ya Ongezeko la Thamani</b>	<b>93.2</b>	<b>93.4</b>	<b>93.4</b>	<b>93.6</b>	<b>93.8</b>	<b>93.7</b>	<b>93.7</b>	<b>91.9</b>	<b>92.2</b>	<b>92.3</b>	<b>93.1</b>
	Ongeza kodi katika bidhaa	6.8	6.6	6.6	6.4	6.2	6.3	6.3	8.1	7.8	7.7	6.9
	<b>Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko</b>	<b>100</b>	<b>100</b>	<b>100</b>	<b>100</b>	<b>100</b>	<b>100</b>	<b>100</b>	<b>100</b>	<b>100</b>	<b>100</b>	<b>100</b>



**PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI**  
(Bei za mwaka 2007)

Jedwali NA.3		<i>Sh. Milioni</i>										
<b>SHUGHULI YA KIUCHUMI</b>		<b>2007</b>	<b>2008</b>	<b>2009</b>	<b>2010</b>	<b>2011</b>	<b>2012</b>	<b>2013</b>	<b>2014</b>	<b>2015</b>	<b>2016</b>	<b>2017</b>
A	<b>Kilimo, Misitu na Uvuvi</b>	<b>7,181,357</b>	<b>7,720,033</b>	<b>8,113,750</b>	<b>8,332,436</b>	<b>8,621,829</b>	<b>8,901,917</b>	<b>9,186,731</b>	<b>9,497,469</b>	<b>9,719,965</b>	<b>9,924,182</b>	<b>10,276,557</b>
	Kilimo cha Mazao	3,603,539	3,884,784	4,098,750	4,248,443	4,454,219	4,640,787	4,801,783	4,993,855	5,106,027	5,175,489	5,365,377
	Mifugo	2,513,284	2,715,826	2,859,665	2,900,642	2,948,017	3,001,944	3,062,481	3,129,647	3,204,928	3,287,499	3,378,129
	Misitu	639,762	663,869	697,692	721,555	745,684	771,590	808,231	849,445	871,448	901,161	957,830
	Uvuvi	424,772	455,555	457,643	461,796	473,910	487,597	514,235	524,521	537,562	560,033	575,222
	<b>Viwanda na Ujenzi</b>	<b>5,406,038</b>	<b>5,759,171</b>	<b>5,949,363</b>	<b>6,489,910</b>	<b>7,271,804</b>	<b>7,566,057</b>	<b>8,287,309</b>	<b>9,144,464</b>	<b>10,174,156</b>	<b>11,265,362</b>	<b>12,626,539</b>
B	Uchimbaji Madini na Mawe	935,412	843,949	1,001,653	1,074,285	1,141,798	1,217,823	1,264,845	1,383,349	1,508,923	1,682,719	1,976,961
C	Viwanda	1,880,032	2,094,035	2,192,207	2,388,391	2,554,119	2,659,200	2,831,400	3,024,323	3,222,077	3,472,664	3,718,853
D	Umeme	232,622	251,361	262,100	297,238	284,394	293,804	332,080	363,110	384,271	416,376	425,339
E	Maji safi na Maji taka	240,898	246,507	257,755	263,336	260,050	267,407	274,507	284,755	285,003	297,151	346,851
F	Ujenzi	2,117,074	2,323,320	2,235,648	2,466,660	3,031,443	3,127,824	3,584,477	4,088,927	4,773,882	5,396,450	6,158,535
	<b>Huduma</b>	<b>12,692,496</b>	<b>13,225,206</b>	<b>13,989,391</b>	<b>15,076,525</b>	<b>16,341,278</b>	<b>17,520,835</b>	<b>18,767,585</b>	<b>20,119,051</b>	<b>21,511,358</b>	<b>23,137,889</b>	<b>24,667,595</b>
G	Biashara na Matengenezo	2,645,347	2,817,146	2,893,444	3,181,783	3,541,265	3,675,197	3,839,852	4,223,837	4,552,422	4,855,513	5,144,531
H	Uchukuzi na Uhifadhi mizigo	1,572,854	1,601,242	1,712,475	1,896,112	1,980,177	2,062,518	2,314,221	2,603,499	2,810,378	3,141,660	3,664,258
I	Malazi na Huduma ya chakula	481,997	497,897	502,992	521,540	543,173	579,598	595,724	609,111	622,966	646,197	667,007
J	Habari na Mawasiliano	615,066	688,106	871,411	1,084,423	1,177,462	1,439,326	1,631,263	1,762,116	1,974,819	2,231,111	2,558,975
K	Fedha na Bima	756,075	898,007	1,062,921	1,197,164	1,374,537	1,445,140	1,534,231	1,699,700	1,900,297	2,103,991	2,145,013
L	Upangishaji Majengo	1,601,266	1,628,117	1,656,750	1,687,264	1,719,706	1,754,126	1,790,574	1,829,107	1,869,782	1,912,659	1,957,802
M	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi	318,677	416,091	481,737	625,810	655,947	617,853	651,358	654,930	699,556	743,797	788,057
N	Huduma zinazohusiana na Utawala	793,110	778,586	781,579	849,168	892,397	1,104,372	1,239,495	1,313,618	1,375,562	1,404,965	1,457,480
O	Utawala na Ulinzi	2,179,164	2,042,643	2,027,532	1,926,209	2,231,564	2,435,459	2,625,280	2,728,183	2,854,132	3,045,808	3,006,479
P	Elimu	851,208	932,429	1,017,818	1,082,540	1,143,385	1,228,099	1,280,673	1,341,507	1,425,992	1,541,076	1,672,411
Q	Afya na Huduma za Jamii	438,415	462,620	497,047	513,696	541,093	602,632	655,861	709,310	742,629	781,589	828,030
R	Sanaa na Burudani	91,527	97,422	100,381	107,674	116,005	128,764	136,162	143,933	152,891	166,415	178,986
S	Huduma nyingine za Kijamii	254,462	269,097	284,963	302,194	320,944	341,382	363,702	388,120	414,881	444,610	476,925
T	Shughuli za Kaya katika kuajiri	93,329	95,802	98,341	100,947	103,623	106,369	109,188	112,082	115,052	118,500	121,641
X	Ushuru wa Mabenki	-331,002	-353,602	-424,177	-457,867	-561,275	-568,183	-568,580	-623,558	-696,521	-810,063	-722,061
	<b>Jumla ya Ongezeko la Thamani</b>	<b>24,948,888</b>	<b>26,350,808</b>	<b>27,628,327</b>	<b>29,441,005</b>	<b>31,673,636</b>	<b>33,420,626</b>	<b>35,673,045</b>	<b>38,137,426</b>	<b>40,708,959</b>	<b>43,517,370</b>	<b>46,848,630</b>
	Ongeza kodi katika bidhaa	1,821,544	1,909,825	2,153,392	2,234,499	2,505,661	2,515,833	2,873,500	3,093,939	3,391,850	3,656,415	3,676,457
	<b>Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko</b>	<b>26,770,432</b>	<b>28,260,633</b>	<b>29,781,719</b>	<b>31,675,504</b>	<b>34,179,297</b>	<b>35,936,459</b>	<b>38,546,546</b>	<b>41,231,365</b>	<b>44,100,809</b>	<b>47,173,785</b>	<b>50,525,087</b>

**PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI - UKUAJI**  
(Bei za mwaka 2007)

Jedwali NA.4		<i>Asilimia</i>										
<b>SHUGHULI YA KIUCHUMI</b>		<b>2007</b>	<b>2008</b>	<b>2009</b>	<b>2010</b>	<b>2011</b>	<b>2012</b>	<b>2013</b>	<b>2014</b>	<b>2015</b>	<b>2016</b>	<b>2017</b>
A	<b>Kilimo, Misitu na Uvuvi</b>	<b>2.4</b>	<b>7.5</b>	<b>5.1</b>	<b>2.7</b>	<b>3.5</b>	<b>3.2</b>	<b>3.2</b>	<b>3.4</b>	<b>2.3</b>	<b>2.1</b>	<b>3.6</b>
	Kilimo cha Mazao	-1.5	7.8	5.5	3.7	4.8	4.2	3.5	4.0	2.2	1.4	3.7
	Mifugo	7.8	8.1	5.3	1.4	1.6	1.8	2.0	2.2	2.4	2.6	2.8
	Misitu	6.0	3.8	5.1	3.4	3.3	3.5	4.7	5.1	2.6	3.4	6.3
	Uvuvi	0.9	7.2	0.5	0.9	2.6	2.9	5.5	2.0	2.5	4.2	2.7
B	Uchimbaji Madini na Mawea	9.2	-9.8	18.7	7.3	6.3	6.7	3.9	9.4	9.1	11.5	17.5
C	Viwanda	11.5	11.4	4.7	8.9	6.9	4.1	6.5	6.8	6.5	7.8	7.1
D	Umeme	18.7	8.1	4.3	13.4	-4.3	3.3	13.0	9.3	5.8	8.4	2.2
E	Maji safi na Maji taka	-7.3	2.3	4.6	2.2	-1.2	2.8	2.7	3.7	0.1	4.3	16.7
F	Ujenzi	13.1	9.7	-3.8	10.3	22.9	3.2	14.6	14.1	16.8	13.0	14.1
G	Biashara na Matengenezo	12.9	6.5	2.7	10.0	11.3	3.8	4.5	10.0	7.8	6.7	6.0
H	Uchukuzi na Uhifadhi mizigo	2.0	1.8	6.9	10.7	4.4	4.2	12.2	12.5	7.9	11.8	16.6
I	Malazi na Huduma ya chakula	4.5	3.3	1.0	3.7	4.1	6.7	2.8	2.2	2.3	3.7	3.2
J	Habari na Mawasiliano	17.7	11.9	26.6	24.4	8.6	22.2	13.3	8.0	12.1	13.0	14.7
K	Fedha na Bima	21.7	18.8	18.4	12.6	14.8	5.1	6.2	10.8	11.8	10.7	1.9
L	Upangishaji Majengo	1.6	1.7	1.8	1.8	1.9	2.0	2.1	2.2	2.2	2.3	2.4
M	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi	12.1	30.6	15.8	29.9	4.8	-5.8	5.4	0.5	6.8	6.3	6.0
N	Huduma zinazohusiana na Utawala	2.1	-1.8	0.4	8.6	5.1	23.8	12.2	6.0	4.7	2.1	3.7
O	Utawala na Ulinzi	9.1	-6.3	-0.7	-5.0	15.9	9.1	7.8	3.9	4.6	6.7	-1.3
P	Elimu	13.2	9.5	9.2	6.4	5.6	7.4	4.3	4.8	6.3	8.1	8.5
Q	Afya na Huduma za Jamii	7.0	5.5	7.4	3.3	5.3	11.4	8.8	8.1	4.7	5.2	5.9
R	Sanaa na Burudani	7.5	6.4	3.0	7.3	7.7	11.0	5.7	5.7	6.2	8.8	7.6
S	Huduma nyingine za Kijamii	5.7	5.8	5.9	6.0	6.2	6.4	6.5	6.7	6.9	7.2	7.3
T	Shughuli za Kaya katika kuajiri	2.7	2.7	2.7	2.7	2.7	2.7	2.7	2.7	2.7	3.0	2.7
X	Ushuru wa Mabenki	11.7	6.8	20.0	7.9	22.6	1.2	0.1	9.7	11.7	16.3	-10.9
	<b>Jumla ya Ongezeko la Thamani</b>	<b>7.1</b>	<b>5.6</b>	<b>4.8</b>	<b>6.6</b>	<b>7.6</b>	<b>5.5</b>	<b>6.7</b>	<b>6.9</b>	<b>6.7</b>	<b>6.9</b>	<b>7.7</b>
	Ongeza kodi katika bidhaa	31.0	4.8	12.8	3.8	12.1	0.4	14.2	7.7	9.6	7.8	0.5
	<b>Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko</b>	<b>8.5</b>	<b>5.6</b>	<b>5.4</b>	<b>6.4</b>	<b>7.9</b>	<b>5.1</b>	<b>7.3</b>	<b>7.0</b>	<b>7.0</b>	<b>7.0</b>	<b>7.1</b>